# PDPC FARAGHA NEWSLETTER

Toleo Na. 0005 Januari - Machi 2026


“Taasisí au mtu yeyote atakayebainika kuendelea na shughuli za ukusanyaji au uchakataji wa Taarifa Binafsi bila kujisajili au kinyume na matakwa ya Sheria na Kanuni zake, atachukuliwa hatua kali za kisheria”

**HABARI KAMILI UK. 03**



Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki,
Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Mb)

## GPSA YAFIKIWA NA PDPC KUHUSU ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Mafunzo hayo yalitolewa tarehe 23 Januari 2026 jijini Dodoma na Bw. Innocent Mungy. **HABARI KAMILI UK. 08**



# YALIYOMO

03 TAASISI ZA UMMA NA BINAFSI ZINAZOKUSANYA NA KUCHAKATA TAARIFA BINAFSI ZIJISAJILI PDPC KABLA YA APRIL 8, 2026.

06 PDPC YATOA DIRISHA LA MWISHO LA USAJILI WA TAASISI ZINAZOKUSANYA NA KUCHAKATA TAARIFA BINAFSI.

07 TAASISI ZOTE NCHINI NI LAZIMA KUWA NA AFISA ULINZI WA TAARIFA.

09 HABARI PICHA.

12 TAB WAISHUKURU PDPC KUWAPATIA ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

13 KUTOTEKELEZA MATAKWA YA PDPA NI HATARI KWA FARAGHA, USALAMA NA HAKI ZA WANANCHI.

17 PDPC YATOA ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA WAFANYABIASHARA MKOA WA NJOMBE.




Waziri wa Mawasiliano na Teknojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (kulia) akikabidhi cheti cha ushiriki kwa mmoja wa washiriki wa mafunzo maalum kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa yaliyofayika mwezi Januari, 2026 jijini Arusha.

# TAASISI ZA UMMA NA BINAFSI ZINAZOKUSANYA NA KUCHAKATA TAARIFA BINAFSI ZIJISAJILI PDPC KABLA YA APRIL 8, 2026.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki, amezitaka taasisi zote za umma na binafsi zinazokusanya au kuchakata taarifa binafsi kuhakikisha zinajisajili Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kabla ya tarehe 8 Aprili, 2026.

Mhe. Kairuki alizungumza hayo wakati wa kufunga mafunzo ya Maafisa wa Ulinzi wa Taarifa, ambapo alisema Serikali imetoa kipindi cha nyongeza cha miezi mitatu kuanzia Januari 8, 2026 hadi Aprili 8, 2026, ili kutoa fursa ya mwisho kwa taasisi ambazo bado hazijatimiza matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kujisajili kwa hiari.

“Serikali imeamua kutoa muda huu wa ziada wa miezi mitatu kuanzia tarehe 8 Januari 2026 hadi tarehe 8 Aprili 2026, ili kuhakikisha hakuna taasisi inayokosa fursa ya kutekeleza wajibu wake wa kisheria. Baada ya tarehe hiyo, utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi utaanza kikamilifu bila msamaha wowote,” alisisitiza Mhe. Kairuki.

Aidha, Waziri aliielekeza Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kuanza mara moja maandalizi ya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, utakaoanza rasmi mara tu baada ya kumalizika kwa kipindi hicho cha nyongeza. Alisema ukaguzi huo utahusisha taasisi, kampuni na watu binafsi wote wanaokusanya, kuhifadhi au kuchakata taarifa binafsi.

**“Taasisí au mtu yeyote atakayebainika kuendelea na shughuli za ukusanyaji au uchakataji wa taarifa binafsi bila kujisajili, au kinyume na matakwa ya Sheria na Kanuni zake, atachukuliwa hatua kali za kisheria bila kusita,” alisema Waziri.**

Wito huo unakuja katika juhudi za Serikali kuhakikisha haki ya faragha inalindwa, usalama wa taarifa binafsi unaimarishwa, na uwajibikaji katika matumizi ya taarifa za wananchi unazingatiwa ipasavyo katika sekta zote.






Baadhi ya Wanachama wa Shirika la Vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Wilaya ya Mafia wakiwa kwenye picha ya pamoja na Mkurugenzi wa PDPC, Ofisi ya Zanzibar Bi. Rehema Abdala (Wapili kutoka kulia aliekaa) mara baada ya kuhitimisha mafunzo maalumu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa wanachama hao.

# SHIVYAWATA MAFIA WAISHUKURU PDPC KUWAPATIA ELIMU KUHUSU DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI.

Wanachama wa Shirika la Vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Wilaya ya Mafia wameishukuru Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa kuwapatia elimu kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Hayo yamesemwa Machi 14, 2026 na mratibu wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa Lizu Mafia, Bw. Selemani Darusi ambapo amesema kundi la watu wenye ulemavu ni muhimu kupata mafunzo haya kwa wakati na ameishukuru PDPC kwa kukubali kuwaunga mkono.

"Tunaishukuru PDPC kwa kuitikia wito wa kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu na ninawaomba wakati mwingine tukileta maombi ya uhitaji wa mafunzo msisite kutusaidia tena. Amesema Bw. Selemani Darusi

Kwa upande wa PDPC, Mkurugenzi wa PDPC ofisi ya Zanzibar, Bi. Rehema Abdala amewasilisha mada mbalimbali zikiwemo chimbuko la dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, maana na aina za Taarifa Binafsi, uanzishwaji wa PDPC sambamba na majukumu yake, bila kusahau Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa watu wenye mahitaji maalum.

Ushiriki wa kwenye mafunzo haya ni sehemu ya PDPC kuhakikisha elimu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inawafikia Wananchi wote nchini ili utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi uzingatiwe na hivyo kuwa na matokeo chanya katika Sekta ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini.




Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia akizungumza na Waandishi wa Habari (Hawapo pichani) kwenye Mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika Machi 26, 2026 jijini Dodoma.

# PDPC YATOA DIRISHA LA MWISHO LA USAJILI WA TAASISI ZINAZOKUSANYA NA KUCHAKATA TAARIFA BINAFSI NCHINI

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imetoa wito kwa taasisi zote za umma na binafsi nchini kuhakikisha zinakamilisha usajili wao kwa hiari ndani ya kipindi cha nyongeza cha miezi mitatu, kuanzia tarehe 8 Januari hadi 8 Aprili, 2026, ili kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44. Hatua hiyo inatekeleza maelekezo ya Serikali yaliyotolewa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb.), tarehe 8 Januari, 2026.

Akizungumza kuhusu hatua hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Emmanuel Mkilia amesisitiza kuwa kipindi hicho cha nyongeza hakimaanishi kusitishwa kwa utekelezaji wa Sheria, bali ni fursa ya mwisho kwa taasisi ambazo bado hazijajisajiri PDPC.

"Kipindi hiki ni dirisha la mwisho la muda wa hiari kabla ya Tume kuanza kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya taasisi zitakazobainika kukiuka Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi," ameeleza Dkt. Mkilia.

Tume pia imetangaza kuwa mara baada ya kumalizika kwa dirisha hilo la hiari, itaendelea mara moja na ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria kwa taasisi zote zinazokusanya, kuhifadhi, kuchakata au kusafirisha taarifa binafsi ndani na nje ya nchi. Ukaguzi huo utalenga kubaini ukiukwaji wa Sheria na Kanuni zake, na wahusika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwemo faini, kifungo au vyote kwa pamoja, sambamba na kulipa fidia kwa waathirika wa uvunjifu wa sheria hiyo.

PDPC inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa uadilifu na weledi ili kulinda taarifa binafsi za watanzania na kujenga mazingira salama ya matumizi ya teknolojia na huduma za kidijitali ikidhamiria kulinda haki ya faragha katika kipindi hiki cha uchumi wa kidijitali unaokua kwa kasi.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Benno Malisa, akifungua mafunzo maalum kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPOs) kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyoandaliwa na PDPC na kufanyika katika ukumbi wa City Park Garden jijini Mbeya, Februari 11, 2026.

# TAASISI ZOTE NCHINI NI LAZIMA KUWA NA AFISA ULINZI WA TAARIFA

Taasisi zote za umma na binafsi nchini zimetakiwa kuhakikisha zinakuwa na maafisa ulinzi wa taarifa (DPOs) ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44.

Hayo ameyasema Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Benno Malisa, Februari 11, 2026 wakati akifungua mafunzo maalum kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPOs) kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yaliyoandaliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kufanyika katika ukumbi wa City Park Garden jijini Mbeya.

"Taasisi zote ambazo hazina Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi ziharakishe kuweka Maafisa hao ili kutekeleza matakwa ya kisheria. Utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 uendane na adhabu kwa watakaovunja sheria hiyo"

"Kutokana na umuhimu wa kulinda faragha za watu nchini, mafunzo haya ni fursa ya kuweka utaratibu wa kuweza kuwapata maafisa ulinzi wa taarifa walio bora na hivyo kurahisisha utekelezaji wa sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi" amesema Mhe. Malisa.

Mhe. Malisa pia amewaomba PDPC licha ya kuwa najukumu kubwa la kutoa elimu na kuhamasisha hizi taasisi kujisajiri PDPC kwa mujibu wa sheria, ni vizuri PDPC iwe na utaratibu wa kukutana na maafisa hao mara kwa mara kwa lengo la kuwaongezea ujuzi juu ya dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Kwa umuhimu wa mafunzo hayo, Mhe. Malisa amewataka wanaopatiwa elimu hiyo kuifanyia kazi mara baada ya mafunzo ili kusaidia jamii kufahamu haki na wajibu wao wa kulinda taarifa zao pia kusaidia taasisi zao kuwa na misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi wanazozitumia.

Mafunzo hayo maalum kwa (DPOs)Maafisa Ulinzi wa Taarifa yamefanyika Februari 11, 2026 ikiwa ni awamu ya Saba ya mafunzo ya namna hiyo na kwa awamu hii yamefanyika jijini Mbeya kwenye ukumbi wa City Park Garden na yalimalizika Februari 13, 2026.



# GPSA YAFIKIWA NA PDPC KUHUSU DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Kuelekea maadhimisho ya Wiki ya Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) iliendesha mafunzo maalumu kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) yakilenga kuimarisha uelewa wa dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi na mawasiliano kwa umma yanayozingatia faragha za wadau wa taasisi hiyo.

Mafunzo hayo yalitolewa Januari 23, 2026 jijini Dodoma na Bw. Innocent Mungy, Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma wa PDPC, kwa niaba ya Tume.

Katika mafunzo hayo, alisisitiza umuhimu wa GPSA kuwa na mifumo salama, madhubuti na inayozingatia matakwa ya kisheria ya ulinzi wa faragha na taarifa binafsi, kutokana na unyeti wa majukumu na taarifa inazozishughulikia.

Maadhimisho ya Wiki ya Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi yalifikia kilele tarehe 28 Januari 2026, ambapo PDPC iliadhimisha wiki hii kwa kutoa elimu kwa wadau na wananchi kuhusu haki ya faragha, wajibu wa taasisi katika kulinda taarifa binafsi, na matumizi salama ya mifumo ya kidijitali.

Wiki ya faragha na ulinzi wa taarifa binafsi inalenga kuongeza uelewa wa umma, kuimarisha uzingatiaji wa sheria, kanuni na kujenga uaminifu katika huduma zinazotolewa na taasisi za umma na binafsi.

Hatua hyo inaakisi dhamira ya PDPC ya kushirikiana na taasisi za umma katika kujenga utamaduni wa ulinzi wa taarifa binafsi, kuongeza uaminifu wa wadau, na kuhakikisha matumizi salama ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa umma katika uchumi wa kidijitali.





**HABARI PICHA**

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb) ameridhishwa na utendaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Ofisi ya Zanzibar na ameahidi kuiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kuwa taasisi zote za umma na binafsi zinazokusanya au kuchakata taarifa binafsi kuhakikisha zinajisajili Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ili kutoa fursa kutimiza matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi sura ya 44.

Mhe. Kairuki ameyasema hayo Januari 26, 2026 alipotembelea Ofisi ya PDPC - Zanzibar na kuzungumza na baadhi ya watumishi wa PDPC ofisi ya Zanzibar.










# CHAVITA WAPEWA ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Jamii ya viziwi jijini Dar es Salaam imetakiwa kuongeza uelewa kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi ili kujilinda dhidi ya uvujaji wa taarifa nyeti, ikiwemo picha za faragha, jambo ambalo limeonekana kuleta hatari kubwa kwa watu wengi wasiokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sheria zinazolinda taarifa hizo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo ya ulinzi wa taarifa binafsi, Mwenyekiti wa CHAVITA Temeke, Bw. Karim Bakari, alisema mafunzo hayo yamewapa washiriki uelewa mpana kuhusu sheria inasemaje juu ya ulinzi wa taarifa binafsi na namna ya kuzilinda.

Alisema jamii ya viziwi imekuwa kwenye hatari zaidi kwa sababu ya kukosa uelewa wa kutosha kuhusu haki na taratibu za kushughulikia changamoto zinazohusiana na taarifa binafsi.

"Tumeelewa majukumu ya tume na sasa tukikumbana na changamoto yoyote tunajua tunapaswa kuanzia wapi kufuatilia ili kupata haki zetu," alisema Bw. Bakari.

Aidha aliongeza kuwa mafunzo hayo yamewapa mwanga mkubwa washiriki na kuwapa uwezo wa kurudi katika jamii na kuwa mabalozi wa elimu hiyo kwa viziwi wengine pamoja na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wake, Bw. Hamidu Rajabu Kimpundu,Mshiriki wa Mafunzo alisema mafunzo hayo yamewasaidia kuelewa walipotoka na wanakoelekea katika suala la ulinzi wa taarifa binafsi nchini.

Alisema kupitia mafunzo hayo wamegundua umuhimu wa kutambua kuwa kuna taarifa binafsi ambazo ni siri kati ya mhusika na mhusika, hivyo si sahihi kuzitoa kwa mtu mwingine ambaye si mhusika wa taarifa hizo.

Mafunzo hayo yamelenga kuongeza uelewa kwa jamii ya viziwi kuhusu haki zao, wajibu wao na hatua za kuchukua pindi taarifa zao binafsi zinapovuja au kutumiwa vibaya na yameandaliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ikiwa ni hatua ya Kutoa Elimu Kwa umma juu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.




Baadhi ya wanachama wa Jumuiya ya Wasioona Tanzania (TAB) wakiwa kwenye ukumbi wa mikutano wa Hotel De Mag jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kushiriki mafunzo elekezi ya siku moja ya kuwajengea uelewa kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

## TAB WAISHUKURU PDPC KUWAPATIA ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Jumuiya ya Watu Wasioona Tanzania (TAB) tarehe 11 Machi, 2026 wamepatiwa mafunzo elekezi juu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kuhakikisha kila mtanzania anaielewa vyema Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kuzingatia utekelezaji wake.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo, mwenyekiti wa Jumuiya ya Watu Wasioona Tanzania Bw. Omary Hamisi Itambo, ameishukuru PDPC kwa kukubali kuendesha mafunzo hayo kwa kuwa ni muhimu sana kwa watu wasioona.

"Tunamshukuru sana Mkurugenzi Mkuu wa PDPC Dkt. Emmanuel Mkilia kwa kukubali ombi letu kuandaa mafunzo haya maalum kwetu. Mmekuja kwa wakati sahihi, tutapata kujua ulinzi wa taarifa binafsi unazingatiwaje hasa kwa watu wenye ulemavu wa kutokuona. Mmetuwezesha kutokuona kwetu kutokuwa sababu ya kuwa nyuma ya mambo ya kitaifa yakiwemo kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa binafsi"

Bw. Itambo pia ametumia nafasi hiyo kumuomba Mkurugenzi Mkuu PDPC kulifanya swala hili la kutoa elimu ya dhana ya

**"Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Mkilia ameenenda sawa na upendo wa Mhe. Rais kwa kuwa aliagiza wasikilizeni watu wenye ulemavu na kutatua changamoto zao na nyinyi PDPC mmeanza kulitekeleza hili"**

Ulinzi wa Taarifa Binafsi hasa kwa watu wasioona kuwa endelevu kwa kuwa waliopatiwa mafunzo haya kwa sasa ni Kundi dogo tu kati ya wengi waliopo nchi nzima.

"Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Mkilia ameenenda sawa na upendo wa Mhe. Rais kwa kuwa aliagiza wasikilizeni watu wenye ulemavu na kutatua changamoto zao na nyinyi PDPC mmeanza kulitekeleza hili"

"Kundi unaliloina hapa ni wawakilishi wa watu wasioona. Naiomba Tume yako tukufu ikubali kuendelea kutoa elimu hii ili kujua haki za taarifa binafsi, ulinzi wake ukoje na faida zake ni nini. Ipo mikoa ya pembezoni, ikikupendeza Katavi, Kigoma, Rukwa na Mbeya wapatiwe elimu hii pia." alisema Bw. Itambo.



Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) akizungumza na Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs), walioshiriki mafunzo maalum ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi awamu ya saba, yaliyofanyika katika ukumbi wa City Park Garden jijini Mbeya, Februari 11, 2026.

## KUTOTEKELEZA MATAKWA YA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI (PDPA) NI HATARI KWA FARAGHA, USALAMA NA HAKI ZA WANANCHI

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia amesema kuwa kutotekeleza matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPA) ni hatari kwa faragha, usalama na haki za wananchi.

Hayo ameyasema Februari 11, 2026 katika mafunzo maalum ya maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi awamu ya saba, yaliyofanyika katika ukumbi wa City Park Garden jijini Mbeya akiwa anazungumza na washiriki hao.

"Tume imebaini baadhi ya taasisi kutokua tayari kikamilifu kutekeleza matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, hususan katika usajili na uteuzi wa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Baadhi ya taasisi zinaendelea kukusanya na kuchakata taarifa binafsi bila kukamilisha matakwa ya kisheria"

"Lengo la mafunzo haya ni kuhakikisha kuwa ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na matumizi ya taarifa binafsi vinafanyika kwa kuzingatia kikamilifu matakwa ya sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi. Hivyo kupitia mafunzo haya tunatarajia kuona mabadiliko ya vitendo katika taasisi zinazoshiriki mafunzo haya" amesema Dkt. Mkilia.

Dkt. Mkilia amesisitiza kuwa PDPC imejipanga kuanza ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria, kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya usajili na uteuzi wa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi, na kuchukua hatua za kisheria pale ambapo kutabainika ukiukwaji.

Mafunzo haya ya siku tatu kwa maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi yamefanyika jijini Mbeya kuanzia Februari 11 hadi 13, 2026 ikiwa ni awamu ya saba ya mafunzo hayo, kwa kipindi hicho yakilenga taasisi za umma na binafsi zilizopo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZA KWA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI, SURA YA 44 BAADA YA UKOMO WA MWISHO WA USAJILI WA HIARI TAREHE 8 APRILI, 2026

**Dodoma – Machi 26, 2026.**

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ikiwa ni Mamlaka ya Kisheria chini ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44, inapenda kuzitaarifu taasisi zote zinazokusanya au kuchakata taarifa binafsi nchini kuwa muda wa usajili wa hiari unafikia ukomo wake tarehe 8 Aprili, 2026.

Itakumbukwa kuwa Serikali ilitoa muda wa kutosha wa kujisajili kwa hiari kwa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi kabla ya kuanza kwa utekelezaji kamili wa Sheria. Muda huo ulijumuisha:

1. Kipindi cha maandalizi cha miezi nane kilichotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa uzinduzi wa Tume tarehe 3 Aprili, 2024 hadi tarehe 31 Desemba, 2024;
2. Nyongeza iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume kuanzia tarehe 1 Januari, 2025 hadi tarehe 30 Aprili, 2025; na
3. Nyongeza ya mwisho iliyotolewa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb.), tarehe 8 Januari, 2026 ambapo aliweka tarehe 8 Aprili, 2026 kuwa muda wa ukomo wa usajili wa hiari.

Fursa hizi zote zililenga kutoa muda wa kutosha kwa taasisi kujipanga kikamilifu katika kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria. Kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44, taasisi zote zinazokusanya au kuchakata taarifa binafsi ili kutoa huduma katika sekta mbalimbali zinapaswa kujisajili. Taasisi na sekta hizo ni pamoja na:

- Taasisi za Serikali (Wizara, Wakala, Mamlaka za Udhibiti, Taasisi na Mashirika pamoja Halmashauri za Miji, Majiji na Manispaa);
- Sekta ya Fedha (Benki, Kampuni na Mashirika ya Bima, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Taasisi za Fedha, Taasisi na Asasi za Mikopo na Watoa huduma za fedha);
- Sekta ya Elimu (Shule zote, Vyuo, Mashirika na Taasisi za Elimu);
- Sekta ya Afya (Hospitali zote, Vituo vya afya, Zahanati, Kliniki za Kibingwa, Maabara na Maduka ya Dawa yaliyosajiliwa kuhudumia wagonjwa kwa kutumia bima);
- Taasisi zake, Taasisi za Kilimo, pamoja na Vyama vya Ushirika.

UK. 1

Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.
@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

# TAARIFA KWA UMMA

Kwa msingi huo, Tume inautaarifu umma kuwa kuanzia tarehe 9 Aprili, 2026 utekelezaji kamili wa matakwa ya Sheria utaanza na yeyote atakayebainika kutozingatia Sheria atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44. Kwa mujibu wa Kifungu cha 60, 61 na 62 cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi hatua hizo zinajumuisha adhabu ya faini isiyopungua Shilingi 100,000 na isiyozidi Shilingi 20,000,000 kwa Mtu Binafsi au kifungo kisichozidi miaka 10 au vyote kwa pamoja; na faini isiyopungua Shilingi 1,000,000 na isiyozidi Shilingi 5,000,000,000 kwa Taasisi kulingana na aina ya ukiukwaji wa Sheria uliofanywa.

Kabla ya tarehe 8 Aprili, 2026, taasisi zote zinatakiwa kuhakikisha kuwa zimetekeleza yafuatayo:

1. Kuteua Afisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Data Protection Officer);
2. Kujisajili Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;
3. Kuandaa na kutekeleza kikamilifu Sera na Miongozo ya ulinzi wa taarifa binafsi;
4. Kuwa na mifumo salama ya ukusanyaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa binafsi; na
5. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za uzingatiaji za kila Robo ya Mwaka kwa mujibu wa Sheria.

Tume inasisitiza kuwa uzingatiaji wa Sheria si jambo la hiari. Mwelekeo wa sasa ni utekelezaji thabiti wa Sheria ili kulinda haki za msingi za wananchi, hususan haki ya faragha na usalama wa taarifa zao binafsi. Taasisi zote zinahimizwa kuchukua hatua za haraka kuhakikisha uzingatiaji kamili ili kuepuka hatua za kisheria zitakazoanza kuchukuliwa bila taarifa nyingine ya ziada.

Usajili wa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa unafanywa kupitia Mfumo wa Usajili na Ushughulikiaji wa Malalamiko (RCMIS) unaopatikana kwenye kiungo cha https://dataprotection.pdpc.go.tz au kupitia wavuti ya Tume ya **www.pdpc.go.tz.**Kwa maelezo zaidi au msaada wa kiufundi, tafadhali wasiliana na Tume kupitia njia zifuatazo za mawasiliano:

Simu: +255753459155, +255718462536, +255744057652, +255736110505, na +255615779070 au Baruapepe: dg@pdpc.go.tz :helpdesk@pdpc.go.tz

**Imetolewa na:**
**Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia**
**Mkurugenzi Mkuu - PDPC**

UK.2

*"FARAGHA YAKO NI WAJIBU WETU"*

**Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania**
**Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.**
@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI



TUFUATILIE KWENYE

# LINKEDIN

@pdpc.tz





Baadhi ya wafanyabiashara Mkoa wa Njombe wakifatilia kwa umakini Mada ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Iliyokuwa ikiwasilishwa na Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Bw. Innocent Mungy (hayupo pichani) wakati wa Mkutano wa Tisa wa Baraza la Biashara Mkoa wa Njombe uliofanyika Februari 17, 2026 katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe.

## PDPC YATOA ELIMU YA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA WAFANYABIASHARA MKOA WA NJOMBE

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imeendelea kuimarisha uelewa wa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa ulinzi wa faragha na taarifa binafsi, wakati wa Mkutano wa Tisa wa Baraza la Biashara Mkoa wa Njombe uliofanyika Februari 17, 2026 katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe.

Akitoa elimu hiyo, Mkuu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano wa PDPC Bw. Innocent Mungy, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu PDPC Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia, amefikisha salamu na pongezi kwa wafanyabiashara wa mkoa huo kwa mchango wao katika kukuza uchumi wa taifa na kuwasisitiza kuwa ulinzi wa taarifa binafsi si suala la kisheria pekee, bali ni msingi wa uaminifu katika biashara za kisasa.

"Haki ya faragha ni haki ya msingi ya binadamu inayolindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na biashara yoyote inayokusanya au kuchakata taarifa binafsi ina wajibu wa kuzilinda kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 ambayo ni sehemu ya mfumo wa sheria pacha tatu za uchumi wa kidijitali zinazojumuisha Sheria ya Miamala ya Kielektroniki na Sheria ya Usalama Mtandao, ambazo kwa pamoja zinajenga mazingira salama na yenye uaminifu kwa biashara na huduma za kidijitali" amesema Bw. Mungy.

Wafanyabiashara hao wametakiwa kuzingatia misingi ya ulinzi wa taarifa, ikiwemo kukusanya taarifa zinazohitajika tu, kuzilinda dhidi ya uvujaji, kuzitumia kwa madhumuni yaliyokusudiwa, na kuwapa wafanyakazi wao elimu kuhusu wajibu wa kulinda taarifa za wateja.

PDPC inaendelea kuwakumbusha wafanyabiashara wote kuwa muda wa nyongeza wa usajili wa hiari kwa taasisi na biashara zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi unaisha tarehe 8 Aprili 2026, na baada ya hapo Tume itaanza ukaguzi wa utekelezaji wa sheria kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali, hivyo watumie muda uliobaki kujisajili, kuboresha mifumo yao ya ulinzi wa taarifa, na kujenga biashara zinazolinda faragha, uaminifu na ushindani katika soko la kisasa la kidijitali.



**HABARI PICHA:**
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Mhe. Balozi Adadi Rajabu (aliesimama) akiongoza Kikao cha nane cha Bodi hiyo ambacho kilipokea na kujadili utendaji kazi wa PDPC kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba, 2025.

Kikao hicho kilifanyika tarehe 13 Machi 2026 katika ofisi za PDPC zilizopo Mtaa wa Moshi, jijini Dodoma.






15"
KODTEC




Huduma kwa wateja:

**+255753459155**
**+255718462536**
**+255744057652**
**+255615779070**
**+255736110505**

Barua pepe:

**helpdesk@pdpc.go.tz**